


Pambazuko

Ukweli Hauna Kutu

Toleo Namba 003

Jumatatu-Julai 25-Agosti 01, 2022

Uk. 13 - Rais Mwinyi ajenga utamaduni mpya Z'bar



Papa Francis akiongoza misa Vatican hivi karibuni (Picha: Remo Casilli/Reuters)

Papa akerwa wanaozusha anajiuzulu

● Asema afya yake bado 'gado'

YALIYOMO



IGP Wambura kakate pesa za 'bangi'
Uk. 2



Makamba mchuzi wa Rostam?
Uk. 8



Kifo dhalili cha Rais Dos Santos
Uk.12

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

IGP Wambura kakate pesa za 'bangi'

UONGOZI wa juu wa Jeshi la Polisi la Tanzania umefumuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan wiki iliyopita - Julai 20.

Sasa Rais Samia amesuka upya uongozi huo kwa kumteua Kamanda Camillius Mongoso Wambura kuwa Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), akichukua nafasi ya Kamanda Simon Sirro, ambaye ameteuliwa kuwa balozi wa Tanzania nchini Zimbabwe. Wambura kabla ya uteuzi huo alikuwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI).

Mabadiliko hayo makubwa yamegusa makamanda wote wa ngazi za juu wa jeshi hilo, huku wengine wakipandishwa vyeo na kupangiwa kazi nyingine.

Kwanza gazeti la Pambazuko linapenda kumpongeza Kamanda Wambura kwa kuaminiwa na Rais Samia na washauri wake wengine, lakini pia kwa upekee tunampa hongera Kamanda Sirro kwa kufanya kazi yake na sasa aende akatumike vyema kuwakilisha nchi.

Wakati tunampongeza Kamanda Wambura, gazeti la Pambazuko linamtia shime ya dhati kwamba tuko bega kwa bega naye kumsaidia kutekeleza majukumu yake mapya, huku tukimtaka kwenda kuangalia maslahi ya askari wa jeshi hilo.

Pia tunampa angalizo la kuwa makini na wengi, hasa baadhi ya wafanyabiashara na wale wanaojitanabaisha wazalendo kwa kutoa misaada ya mali kwa jeshi hilo.

Wengi wa hawa, taarifa zinaonyesha wamekuwa chanzo cha 'kulainisha' viongozi wa juu wa taasisi zetu ili mambo yao yanyooke na kutoguswa hata pale wanapobainika kwamba ni wauza 'bangi.'

Katu hatukatai misaada kutoka kwa wasamaria na wazalendo wa kweli wanaofanya shughuli zao halali, kusaidia popote, lakini tunalaani kwa nguvu zote fedha za dawa za kulevywa na 'ushetani' mwingine kutumika kusaidia majeshi yetu au taasisi za serikali. Ni laana.

Ni misaada ya aina hiyo imekuwa ikilifanya jeshi letu kuonekana dhalili mbele ya wafanyabiashara hao na kutamba pale wanapokamatwa na askari - wasiokuwa maofisa, kwa 'kuwavimbia' na kuwatukana - kwa kuwa tu wanajuana na wakubwa. Tunahitaji heshima kwa jeshi letu.


Pamoja na hilo, tunamtaka Kamanda Wambura kwenda kusafisha baadhi ya askari wasiokuwa na weledi, wanaobambika watu kesi, kuwatesa wanapowakamata na kudhalilisha utu wao. Hili limekuwa sugu mno ndani ya jeshi hilo la Polisi.

Sambamba na hilo, Kamanda Wambura akalifanye jeshi liwe mahali salama pa kila mwananchi kwenda kuhudumiwa bila kulazimishwa kutoa rushwa au kukandamizwa.

Katika miaka ya hivi karibuni, rushwa imeonekana kuwa 'huduma' ya kawaida ndani ya jeshi hilo kwa kuwa hata baadhi ya wakubwa wanadaiwa kuwa na ukwasi mkubwa - ambao bila shaka unatokana na rushwa hiyohiyo.

Hivi inakuwaje kiongozi wa jeshi anakuwa na nyumba za kisasa kila mkoa? Amepata wapi pesa hizi kama siyo rushwa? Hatutarajii Kamanda Wambura kuwa hivyo.

Kila jema kwa Kamanda Wambura na timu yake.



Jisajili kupata Pambazuko bure

Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** na kutuma neno “**HABARI**” ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

Pia unaweza kujisajili kwa kutumia Email hii: **pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno “**HABARI**” na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Tubadili sura, muundo, sheria au tuanzishe upya Jeshi la Polisi?

Na Plato Hekimachius

RAIS Samia Suluhu Hassan amefanya mabadiliko ya uongozi wa juu wa Jeshi la Polisi. Hotuba yake siku ya kua-pisha wakuu wapya, inaashiria mabadiliko, lakini uteuzi alioufanya unaashiria mwendelezo wa “mambo” ya polisi.

Walioondoka na walioingia ni walewale. Huu ni mvinyo wa zamani katika chupa mpya. Naweza kusema hawa walioteuliwa – kuanzia mkuu mpya wa jeshi hilo na wengine wote ni makamanda waliorithiwa kutoka awamu iliyoipita, chini ya Rais John Pombe Magufuli. Hawa wanabeba sifa na zaidi tuhama zilizokuwepo wakati huo, hasa za kuminya haki za binadamu.

Swali la msingi ni je Rais Samia aanzie wapi katika mabadiliko anayoyaahidi?

Marais wote waliopita walibadili sura ili kuleta ufanisi ndani ya jeshi hilo. Mmoja alibadili sheria na kulifanya jeshi lijikite katika intelijensia na utii wa sheria bila shuruti.

Ili kuleta mabadiliko yanayotarajiwa Rais Samia aangalie haya sambamba na muundo wa sheria.

Kwanza, aondoe kinga ya kuwashtaki makamanda wanaofanya vitendo vya jinai. Makamanda wengi wanaogelea katika utajiri mkubwa usio na maelezo. Hii ni karibu kwa vyombo vyote vya ulinzi, lakini Jeshi la Polisi ni zaidi. Wengi wao wana makumi ya nyumba za kupanga (estates), magari, mashamba makubwa na biashara za mafuta. Utajiri mkubwa kwa makamanda wa vikosi vya ulinzi ni hatari kwa serikali.

Pili, Rais Samia aache kuwateua makamanda katika nafasi za kiraia. Huu utaratibu wa kuwateua kuwa mabalozi, wakuu wa mikoa na makatibu wakuu wa wizara ni kusambaza kansa ya rushwa katika maeneo wanakopelekwa.

Tatu, Rais Samia aanzishe mchakato wa



IGP Wambura

kutunga sheria ya kuwazuia makamanda wa majeshi yetu kutojihusisha na siasa baada ya kustaafu kwa muda wa miaka mitano mpaka 10. Wengi wao wanakimbilia huko kulinda maslahi yao.

Nne, Rais Samia asitische mara moja utaratibu wa sasa wa IGP kuteua makamanda wa mikoa na wilaya na kiwepo chombo maalum ndani ya jeshi kufanya kazi hiyo. Utaratibu wa sasa unawezesha mitandao ya kisiasa, rushwa na uhaini-baridi.

Tano, Rais Samia akomeshe muingiliano wa utendaji wa vyombo vya usalama kwa sababu vinaweza kabisa kunachafuana. Mfano hakuna sababu ya Polisi kukamata halafu chombo kingine cha usalama kikaja kuhoji na hata kutesa vituoni mwa Polisi. Hii siyo sawa.

Waziri Makamba ‘apangua’ kuitwa mchuuzi wa Rostam

Na Mwandishi Wetu

MITANDAO ya kijamii; hasa Twitter, Facebook na makundi ya WhatsApp wiki iliyoisha jana, yalitingwa kwa madai kwamba Waziri wa Nishati, January Makamba amegeuka kuwa mchuuzi wa moja ya bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya mfanyabiashara maarufu, Rostam Aziz.

Bidhaa iliyozungumzwa ni mitungi ya gesi asilia inayotumika majumbani ya Taifa Gas.

Katikati ya mwezi huu, Waziri Makamba alianza ziara ya mikoa 14 na wilaya 38 ikiwa na lengo la kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini.

Waziri Makamba katika ziara hiyo, anapozungumza na wananchi kuwaeleza namna serikali ilivyojipanga kuondoa matumizi ya kuni na mkaa, anagawa mitungi ya gesi akieleza kuwa na nia ya kuwafunza na kuwapa msukumo kutumia nishati hiyo mbadala isiyokuwa na madhara makubwa kwa mazingira na afya za binadamu.

Takwimu zinaonyesha kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazotumia mkaa na kuni kwa wingi katika Afrika, huku madhara yake yakirekodiwa kusababisha vifo 22,000 kila mwaka nchini kutokana na magonjwa ya njia ya kupumua yanayosababishwa na matumizi ya kuni na mkaa. Pia ukataji miti kwa wingi kunasababisha jangwa na “kuikimbiza” mvua.

Pamoja na kueleza faida nyingi za matumizi ya gesi na namna serikali ilivyojipanga kuhimiza matumizi ya nishati hiyo, ikiwamo kupunguza kodi, bado wananchi - kwa uhuru wa kutoa maoni walionao, wamekuwa wakipaza sauti kupitia mitandao ya kijamii na kuhoji; je, kwanini Makamba haelezi endapo serikali inanunua mitungi hiyo na kugawa bure; je, ni mpango endelevu? Je, mitungi hiyo inapatikana jirani endapo



Rostam Aziz

waliopewa wataishiwa gesi? Kwanini iwe ni mitungi ya Taifa Gesi pekee na maswali mengine.

Mtu mmoja kwenye mtandao wa Twitter anayejiita Zee la Jiji anasema katika uzi wa maswali haya kwamba – “Makamba ni waziri makini, namuomba asijibu upuuzi huu na aachwe afanye kazi.”

Akiwa Karagwe, mkoani Kagera, Waziri Makamba aliwajibu wanaoibua maswali hayo kwamba serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan imejipanga kupunguza kero ya nishati yenye madhara.

Waziri Makamba anasema kamwe hafanyi siasa katika kuhakikisha nia ya Rais Samia ya kupunguza madhila na kero kadhaa za nishati inafanikiwa bila kujali kinachosemwa mitandaoni kwa lengo la kukatisha tamaa.

Mchangiaji mwingine kutoka mtandao wa Twitter akijiita Calito anaandika – “Vita anayopigwa Makamba kwenye mitungi ya gesi, siyo yake, bali ni washindani wa Rostam katika biashara ya nishati hiyo. Hawa wajipange – kwani Rostam anaona mbali.”

Hapa na Pale

6

Washington

Biden ana ugonjwa wa kusahau?

AFYA ya Rais wa Marekani, Joe Biden inaendelea kuzua minong'ono ndani na nje ya nchi yake baada ya kuonekana hadharani "akisahasahau" katika kauli zake.

Rais Biden (79), kiongozi wa 46 wa Marekani amekuwa akisikika kutamka maneno ambayo ni kinyume na hali halisi. Hali hiyo inatafrisiriwa kuwa ni ugonjwa unaotokana na uzee.

Mfano ni Jumatano iliyopita – Julai 20 akiwa huko Somerset, Massachusetts, Marekani aliposema "nina kansa." Ikulu ya nchi hiyo harakaharaka ikafafanua kwamba alikuwa akirejea ugonjwa huo zamani- lakini kwa sasa amepona.

Pia hivi karibuni amewahi kumtambulisha makamu wake, Kamala Harris kuwa ni 'first lady' (mkewe). Pia Ikulu ya nchi hiyo ikaleta ufafanuzi haraka.

- Mashirika

Malawi


Padre muuaji wa albino afia gerezani

PADRE wa Kanisa Katoliki Jimbo la Zomba nchini Malawi, Dkt. Thomas Muhosha (50), amefariki dunia Jumanne iliyopita – Julai 19, 2022.

Taarifa iliyotolewa wiki iliyopita na Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Malawi zinaeleza kuwa Dkt. Muhosha wakati akiendelea na matibabu katika Hospitali ya Zomba.

Padre huyo alisimamishwa kutoa huduma za kiroho na Kanisa Katoliki baada ya kupatikana na hatia ya kuua watu wenye ulemavu wa ngozi (albino) na kufanya biashara ya viungo vyao. Alikuwa akitumikia kifungo cha miaka 30 jela.

-UCA



Rais wa Marekani, Joe Biden

India

Maji machafu yamlaza hospitali waziri mkuu

WAZIRI Kiongozi wa Jimbo la Punjab, India, amelazwa hospitalini baada ya kunywa maji yanayoaminika kuwa "matakatiifu."

Kiongozi huyo, Bhagwant Mann, alilazwa Alhamisi iliyopita – Julai 21, 2022 katika Hospitali ya Indraprastha Apollo, iliyoko Delhi, siku mbili baada ya kuonekana akinywa maji ya Mto Kali Bein, yanayoaminika kuwa matakatiifu kwa jamii ya Masingasinga.

Masingasinga wamekuwa wakinywa na kuoga maji ya mto huo, wakiadini kuwa wanatakaswa dhambi zao na kuwaletea afya, bahati na kupunga upepo mbaya.

Chama cha siasa cha kiongozi huyo, AAP kimekanusha habari kwamba waziri kiongozi aliugua baada ya kunywa maji hayo, lakini kimekiri kwamba alikwenda hospitali kwa uangalizi wa afya yake.

-Hindustan

Ruto: Nashindana na serikali, Uhuru, Raila na familia zao

Na Mwandishi Wetu, Nairobi

WILLIAM Ruto, mgombea urais wa Kenya katika uchaguzi mkuu mwaka huu – 2022 unaofanyika Agosti 9, unaendelea kuwapa nafasi wapigakura kuwatambua vyema wagombea wao.

Jana Jumapili, Ruto ambaye ni Naibu Rais wa Kenya ameambia Pambazuko kwamba ana uhakika mwa kuibuka mshindi kwa kuwa nguvu kubwa iliyowekwa na mgombea mwenzake, Raila Odinga ameishinda tayari.

“Mimi nimeshinda, nasubiri tu kuapishwa kwa kuwa sioni mshindani wangu akipata ushindi kwa njia yoyote ile, ushindi wangu uko wazi na hakuna asiyeuona ukija,” anatamba Ruto.

Ruto anadai kwamba nguvu kubwa ya mgombea mwenzake Raila haiwezi kufua-dafu kwani hesabu zimepigwa na zinaonyesha yeye ni mshindi kwa mbali.

“Nguvu ya Raila imekuwasanya kundi kubwa sana la watu wenye nvugu, akiwamo Rais Uhuru Kenyatta, serikali yake na familia zao - na Raila na familia yake, hawaniwezi kwani Wakenya wameamua,” anaongeza Ruto akionekana mwenye imani ya kushinda.

Katika hatua nyingine, Ruto anadai kwamba yeye alishiriki kumuweka Uhuru kwenye madaraka ya urais, lakini baadaye amengeuka na kuwa upande wa mpinzani wake.

Ruto anadai kwamba Rais Uhuru alikubaliana na kuahidi kumpigania makamu wake ili awe kiongozi wa Kenya baada ya kumaliza muda wa kuongoza nchi hiyo ya Afrika Mashariki.

Alipoulizwa na Pambazuko endapo walikubaliana kwa maandishi (kufunga mkataba), Ruto alidai walikubaliana kwa mdomo na kuwa Rais Uhuru aliwahi kutamka hadharani kuhusu ahadi hiyo.

Ruto anadai kwamba hata bila nguvu ya ushawishi wa Rais Uhuru, hana wasiwasi kwa ushindi wake – kwani



Mgombea urais wa Kenya, William Ruto

Wakenya wameamua kuachana na kukumbatia majina ya familia kubwa nchini humo.

Uchaguzi wa Rais wa Kenya, pamoja na kuwa na wagombea wanne, ni wagombea wawili tu; Raila na Ruto ndiyo wanaopewa nafasi kubwa ya mmoja wao kuibuka na ushindi.

Ruto aliwahi ‘kuonja’ urais wa Kenya kwa siku moja Oktoba 6, 2014 baada ya kuachiwa nafasi hiyo na Rais Kenyatta ambaye alilazimika kwenda nje ya nchi kuhudhuria kesi katika Mahakama ya Kimataifa dhidi ya Makosa Uhalifu (ICC). Kenyatta na Ruto wote walikuwa na kesi katika mahakama hiiyo kufuatia machafuko wakati na baada ya uchaguzi mkuu wa nchi hiyo mwaka 2007/08. ICC ilifuta shauri lao.

Katiba ya Kenya inatoa mwanya wa vipindi viwili – vya miaka mitano kwa kila kiongozi wa nchi hiyo kuwa madarakani na baada ya hapo, uchaguzi mpya hufanyika.

Zimebaki siku 15 Wakenya kuamua

Maendeleo: Divai mpya katika vibuyu vikukuu

Na Askofu Dkt. Stephen Munga

MAENDELEO yamekuwa kichocheo cha juhudi za kufanya kazi kwa kila mtu (mwenye uwezo wa kufanya kazi) katika jamii. Huo ni mtazamo wa upande mmoja. Upande mwingine ni kuwa maendeleo yalitakiwa kuwa kichocheo cha utendaji mzuri katika siasa na uongozi.

Maendeleo katika mjadala huu unasimama katika uelewa wa maendeleo kama mchakato wa kuleta mabadiliko chanya kuelekea hali njema ya maisha ya watu. Hivyo mabadiliko hayo chanya kwa kila mtu, ndio huleta mabadiliko mapana ambayo huwa kipimo cha maendeleo ya jamii kwa ujumla.

Miongoni mwa kauli za kihenga juu ya maendeleo ya jamii ni kauli ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere kuwa ili kuendelea tunahitaji mambo matatu: watu; siasa safi; na uongozi bora. Kauli hii ilikusudiwa kueleweka, kufikirisha na ikiwezekana, kuhojiwa kwa kuuliza maswali zaidi.

Ileweke kwamba mambo hayo hayakutajwa kama kauli za kukaririwa tu, bali ni magurudumu kuelekea maendeleo. Kwa hiyo ni muhimu kila moja kupata uchambuzi wa kina na kufanya yaonekane na kushikika ili kuleta maendeleo halisia.

Kufanya uchambuzi wa kauli hii kongwe na kujaribu kuleta maana kwa wakati wetu ni sawa na kutia divai mpya kwenye viriba vya zamani. Tutaona ikiwa katika kufanya hivyo kutapasua viriba. Wakati huohuo kwa msomaji atamua iwapo juhudi hizi ni sawa na kutia divai ya kale katika viriba vipya. Mwisho wa mjadala huu kila msomaji atajua matokeo ni yapi.

Mimi ni muumini wa mtazamo kuwa maendeleo ya jamii hupimwa kwa ubora wa maisha ya watu katika jamii. Kwa maneno mengine, maendeleo yanafanya



Rais Samia Suluhu Hassan

watu kuwa na makazi mazuri, lishe bora, mavazi, elimu bora kwa watoto na vijana, huduma bora ya afya kwa watu wote, haki sawa kwa wote, uhuru wa kujieleza na kuishi pasipo kuingilia/kuharibu uhuru wa watu wengine na mambo mengine.

Kauli hiyo kwamba watu, siasa safi na uongozi bora ndio magurudumu ya maendeleo inakusudia kuonyesha kwamba maendeleo huletwa na kulindwa kwa utendaji mzuri wa magurudumu hayo matatu. Kwa maneno mengine tunapojiweka vigezo vya kupima maana ya maendeleo ni muhimu pia kujenga vigezo vya magurudumu hayo.

Kwa hiyo tutajishughulisha na kuchambua ni nini na ipi ni nafasi ya watu; nini maana ya siasa safi; na nini maana ya uongozi bora? Kwa uchambuzi huo tutaweza kupima hivyo katika mazingira yetu na kuweza hata kupima kiwango cha maendeleo. Kwa hiyo hatua tuliyofikia kimaendeleo inaweza kueleza aina ya watu tulionao, aina ya siasa yetu,

Itaendea toleo lijalo...



Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com

Mezani kwa Chahali

Wambura, Kingai wasilaumiwe

WIKI iliyopita, Rais Samia Suluhu Hassan alifanya mabadiliko kwenye uongozi wa juu wa Jeshi la Polisi. Katika mabadiliko hayo, Camillius Wambura aliteuliwa kuwa mkuu mpya wa jeshi hilo (IGP), akichukua nafasi ya Simon Sirro aliyeteuliwa kuwa balozi wa Tanzania huko Zimbabwe.

Kadhalika, Ramadhan Kingai aliteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), akichukua nafasi iliyokuwa ikishikiliwa na Wambura.

Japo kulikuwa na watendaji wengine wa jeshi hilo walioguswa na mabadiliko hayo, teuzi zilizogusa hisia za wengi ni huo wa IGP mpya Wambura na DCI mpya Kingai.

Na yayumkinika kuhitimisha kuwa wengi wa walioongelea teuzi hizo za Wambura na Kingai walizikosoa. Baadhi ya waliokosa teuzi hizo walidai kuwa watendaji hao wa Jeshi la Polisi walikuwa sehemu ya madhila yaliyokithiri, hasa ukiukwaji wa haki za binadamu katika awamu iliyopita chini ya Rais John Magufuli.

Kwa upande wa Wambura, baadhi ya walioongelea kuteuliwa kwake, walishangaa kuona IGP mpya akitoka Mkoa wa Mara kama mtangulizi wake. Walieleza kuwa kwa vile Tanzania ina mkoa 25, haipendezi kuona ma-IGP wawili mfululizo wakitoka mkoa mmoja.

Hata hivyo, katika hilo la IGP Wambura na DCI Kingai kuhusishwa na yaliyojiri katika utawala uliopita, binafsi kama mtumishi wa zamani wa chombo cha dola, naweza kuwatetea kwamba “walikuwa wakitekeleza amri halali.”

Kwa mujibu wa taratibu za utumishi katika vyombo vya dola, “amri haihojiwi.” Kwa hiyo bila kujali amri waliopewa watendaji hao zilikuwa halali au la, hawakuwa na nafasi ya kuzigomea.



Ramadhan Kingai

Wakati hisia za wengi zilielekezwa kwenye teuzi hizo, hatua muhimu iliyochokuliwa na Rais Samia – kuunda kamati ya watu 12 na sekretarieti ya watu watano kwa ajili ya kufuatilia utendaji kazi wa vyombo vya ulinzi na usalama nchini humo – haikupata mapokeo stahili.

Hatua hiyo ni muhimu kwa sababu binafsi nimekuwa miongoni mwa sauti adimu ambazo kwa miaka kadhaa zimekuwa zikihimiza umuhimu wa kuwa na uangalizi kwenye utendaji kazi wa vyombo vya ulinzi na usalama. Kwa kimombo wanaita “oversight.”

Japo ufanisi wa kamati na sekretarieti hiyo utategemea zaidi utendaji kazi wake, sambamba na mazingira ya kisheria ya kulazimisha ushirikiano kutoka kwa taasisi husika, uamuzi tu wa Rais Samia kuunda vyombo hivyo ni hatua ya kutia matumaini na inayostahili pongezi.

Shime Rais Samia na timu yako. Sasa kazi kubwa kwa makamanda – katika nafasi mpya, wakafanye kazi kwa haki na utu.

Papa akerwa wanaozusha anajiuzulu



**Papa
Benedict**

Na Tryruckia Mfinanga

KUENDELEA kutetereka kwa afya ya Mkuu wa Kanisa Katoliki Duniani (RC), Papa Francis kumezua wasiwasi endapo bado ana nguvu za kuliongoza kanisa hilo kubwa duniani.

Afya ya Papa Francis (85) katika siku za hivi karibuni imeelezwa na hata kuthibitika hadharani kwamba ina changamoto baada ya kuonekana mara kadhaa akishindwa kunyanyuka kwenye kiti, kushindwa kutembea vyema, kusinzia anapokuwa kwenye hadhira na hata kujongea kwa kutumia baiskeli ya wagonjwa.

Zipo taarifa za ndani kwamba upo mvutano kwenye uongozi wa kanisa hilo unaovutana kuhusu kumuomba Papa Francis aamue kuachia ngazi, huku wengine wakiamini katika utaratibu uliozoeleka wa kumwacha Papa apumzishwe kwa kifo au hata afya ‘kugoma’ kabisa.

Inadaiwa kuwa wasaidizi wake wa karibu wamekuwa na maoni kwamba ni vyema Papa Francis akapumzika mapema kuliko kusubiri afya ikashindwa

kumruhusu kuendelea na majukumu makubwa ya kuliongoza kanisa hilo linaloaminika kuwa na waumini wanaofikia bilioni 1,329 duniani kote kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2020 iliyotangazwa na Kitabu cha Kipapa kuhusu idadi ya waumini (Census of the 2020 Annuario Pontificio).

Katika kuupa mtazamo kwamba Papa Francis – kwa kundi ambalo linaamini ni muda muafaka kwake kupumzika, linadai kuwa kiongozi huyo alishindwa kuanza ziara ya nchi kadhaa, ikiwamo mji jirani kabisa ulioko Italia.

Hata hivyo, pamoja na hoja ya kumuomba Papa Francis kujiuzulu, bado wapo wanaoamini anaweza kuendelea na kazi zake, kwani hajafikia hatua ya “kulala kitandani.”

Uongozi wa kanisa hilo kutoka Vatican, umekuwa ukieleza kwamba afya ya Papa Francis ni “imara na kwamba bado ana uwezo wa kuendelea na kazi zake, isipokuwa tu anasumbuliwa na maumivu ya goti ambayo yanapona haraka.”

Kukomaa kwa uvumi huo kunakolezwa na kuwepo mkutano mkubwa wa makadinali unaofanyika baadaye mwezi

Papa akerwa wanaozusha anajiuzulu

Agosti, 2022 ambapo, pamoja na mambo mengine, utakuwa na agenda ya kujadili Katiba ya RC kwa mazingira ya sasa.

Wapo wanaodai kwamba mkutano huo pia utatumika na Papa Francis kutangaza kuachia ngazi, ingawa wengine ndani ya Vatican wamekanusha jambo hili.

Kutokana na uvumi wa kutetereka kwa afya ya Papa Francis na ushawishi wa kujiuzulu, aliamua kuweka hadharani msimamo wake kwa kuzungumza na Reuters, chombo cha habari cha Reuters – Julai 2, 2022 na kueleza bayana kwamba – “hoja ya kujiuzulu haiko kichwani mwangu kabisa.”

Papa Francis anaeleza kwamba endapo atalazimika kujiuzulu kwa sababu za kiafya, atafanya hivyo, lakini siyo kulazimishwa na watu tu.

Julai mwaka jana – 2021, Papa Francis alifanyiwa upasuaji wa utumbo mkubwa na kulazwa kwa siku 10.

“Ikiwa Mungu ataamua nijuzulu kwa sababu za afya yangu kuzorota, wala sitasita - na siyo kwa kuwasikiliza watu, bali afya imekataa, nitajiuzulu,” anaongeza Papa Francis akizungumza na Reuters huko Vatican.

Papa Francis wakati akizungumza na mwandishi wa Reuters, alionekana akitembea kwa kutumia fimbo, ambapo alisema alishauriwa na madaktari kufanya hivyo kabla ya kuanza kutembea mwenyewe bila msaada.

“Hivi sasa unaona natembea kwa msaada wa fimbo, lakini nafanya hivyo ili kuzuia misuli yangu kushindwa kufanya kazi sawasawa ikiwa nitakaa kwa muda mrefu kitandani au kutumia baiskeli ya wagonjwa, lakini hali yangu ni nzuri,” anaongeza Papa Francis.

Papa Francis pia alitumia mwanya wa kuzungumza na Reuters kwa kupuuzua uvumi mwingine juu ya afya yake kwamba aligundulika kuwa na kansa (saratani) – kwa kusema kwamba; “wapuuzwe wanaoeneza uvumi huo.”

Alisema kwamba aliahirisha ziara yake Sudan Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kwa ushauri wa daktari kwamba alitakiwa kupumzika zaidi na wala haikuwa kwa sababu ya “kuumwa zaidi.”

Katika mazungumzo yake ya dakika 90 (saa moja na nusu) na Reuters, alitumia fursa hiyo kuendeleza msimamo wake wa kupinga utoaji wa mimba, akieleza kwamba kushabikia hatua hiyo ni “kujiptosha pakubwa.”

“Ninashangaa uamuzi wa Mahakama ya Juu ya Marekeni kuidhinisha watu kutoa mimba, ni hatari sana na pia ni chukizo kwa Mungu. Watu waache tabia hii ili kujiepusha na adhabu kubwa ya Mungu,” anaongeza Papa Francis katika mazungumzo hayo aliyoyafanya bila kuwepo msaidizi wake yeyote.

Padre mmoja kutoka Kanisa Katoliki Bunju Dar es Salaam, Parokia ya Bikira Maria wa Mlima wa Karmeli ameliambia Pambazuko kwamba Papa kujiuzulu siyo dhambi na kamwe siyo kosa, na kuhoji – “kwani nguvu za kutenda kazi zikiisha unafanyaje? Huwezi kutumika, unatakiwa kupumzika.”

Akikataa kuandikwa jina kwa kuwa hajui mzizi wa habari inayoandikwa na Pambazuko (pamoja na kufanuliwa), alisema endapo Papa Francis ataamua kujiuzulu, haitakuwa mara ya kwanza kwa kiongozi wa juu wa RC kuondoka madarakani kwa sababu za afya.

Anasema kwamba miaka 600 iliyopita – kwa mara ya kwanza Papa aliamua kuachia majukumu yake ya kuongoza RC na alikubaliwa na Vatican, lakini pia mwaka 2013, Papa Benedict XVI aliachia uongozi kwa hiari yake akiwa na miaka 85 kama aliyonayo sasa Papa Francis. Papa Benedict sasa ana miaka 95.

Mwandishi wa muda mrefu wa masuala ya Kanisa Katoliki anayeishi Vatican, Giovanna Chirri anesema hatua ya Papa kujiuzulu siyo kitu cha kushangaza, anaweza kufanya hivyo kwa imani kwamba hataweza kutekeleza majukumu yake vyema.

Majukumu makubwa ya Papa katika RC ni pamoja na kuhakikisha kanisa hilo linaimarika wakati wote kwa kuwa na waumini watiifu, yeye ni mkuu wa Vatican – hivyo kazi yake ni kujenga uhusiano imara na wakuu wa nchi zingine (Vatican City ni mji wenye hadhi ya nchi), kuteua makadinali na mambo mengine ya kiimani.

Kifo dhalili cha Rais Dos Santos

Na Cláudio Silva

ASILIMIA 73 ya idadi ya watu milioni 33 wa Angola, wameshuhudia utawala wa Rais Jose Eduardo dos Santos, aliyedumu madarakani kwa karibu nusu ya maisha yake – miaka 38. Alizaliwa Agosti 28, 1942 na kufariki dunia Julai 8, 2022. Alikuwa na miaka 80.

Katika kipindi cha utawala wake – 1979 hadi 2017, Rais Dos Santos alikuwa akionekana kila mahali; picha yake kwenye noti, mabango ya kumsifu kila barabara, akisikika kwenye redio na kuonekana kwenye televisheni, hata kama hana kitu cha maana kuwaambia wananchi wake.

Pamoja na kuonekana yupo kila mahali, aligeuka kuwa katili kupindukia, akifunga, kutesa na hata kuuu wale waliioonekana kupinga uongozi wake. Aliwatesa na kuwafunga waliokutwa wakisoma baadhi ya vitabu na majarida ambayo hakupenda kuyaona yakisambazwa Angola. Hakutaka wananchi wake wamjadili kwa mabaya yake. Alipenda sifa na alihakikisha anaongoza kwa mkono wa chuma.

Hata hivyo, pamoja na mbwembwe na “kujimwambafai,” Dos Santos alikufa kitandani peke yake, akiwa uhamishoni huko Barcelona, Hispania.

Angeweza kufa shujaa endapo angeachia madaraka kabla ya uchaguzi wa mwaka 2008 - kwani alikuwa bado na sifa nzuri ya kuwa kinara kwa kumaliza vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini Angola. Rais Dos Santos alileta amani ndani ya jeshi la nchi hiyo, hasa baada ya kuajiri waliokuwa askari wa jeshi la msituni lililokuwa likipinga utawala wake.

Kama angeondoka madarakani kabla ya uchaguzi wa 2008, angewekwa katika historia ya Afrika kama kiongozi mwenye uwezo, ambaye aliongoza nchi kwenye uchumi wa soko la juu duniani.

Sababu za kukengeuka kwa Dos



Rais Jose Eduardo dos Santos,

Santos hazieleweki vyema, lakini wachambuzi wa siasa wanadai huenda ni hasira za kupata chini ya asilimia 50 ya kura zilizopigwa na kumpita kwa kiasi kidogo Jonas Savimbi, aliyekuwa muasi na mpinzani wake kabla.

Baada ya uchaguzi kurudiwa, Dos Santoa alishinda na hapo akageuka kutoka kiongozi bora na kuwa wa hovy; akichagua ufisadi badala ya maendeleo ya watu na nchi yao.

Hata hivyo, pamoja na yote hayo, aliondoka madarakani. Kuondoka kwake madarakani, mambo yakageuka. Raha alizokuwa akiponda na familia yake zikawa shubiri. Watoto wake waliokuwa na utajiri wa kutisha, sasa wanakabiliwa na kesi za ufisadi mahakamani na mwingine amefungwa miaka mitano jela. Fedha zake nyingi alizowekeza kwenye kampuni kadhaa sasa zina mgogoro na huenda familia yake ikazikosa, kwani hakuna mikataba ya kueleweka kati yake na wafanyabiashara hao.

- Habari hii iliyohaririwa ilichapishwa kwa mara ya kwanza na gazeti la The Continent la Afrika Kusini. Unaweza kusoma gazeti hilo kwa kujisajili kwa namba ya WhatsApp kwenda namba +27 73 805 6068.

Rais Mwinyi ajenga utamaduni mpya

Na Jabir Idrissa, Unguja

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi mwenye miaka miwili kasoro ya kuongoza serikali, najenga utamaduni mpya wa uwajibikaji kwa kuchukua hatua ngeni ndani ya visiwa hivyo.

Haikuwahi kutokea kabla ya kuingia kwake madarakani Oktoba 2020, kiongozi wa wadhifa wake kufukuza mkandarasi kwa sababu ya kutowajibika sawasawa.

Kama hiyo haitoshi, haijapata kushuhudiwa Rais wa Zanzibar akiagiza mamlaka ya kupambana na rushwa ya Zanzibar kuchunguza utaratibu uliotumika kutoa kandarasi kwa kampuni.

Wala siyo kwamba hakukuwa na matatizo au kasoro kwenye hatua za utoaji wa zabuni kwa makandarasi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Hapana! Ipo mifano ya uharibifu wa miradi hadi kufikia waliokuwa wakifadhili, kugomea au kujitoa mpaka masharti fulani yatumizwe.

Kwa mfano, mradi wa upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Karume, Zanzibar ulisita kwa zaidi ya miaka mitatu baada ya wafadhili kujitoa kugharamia kwa sababu walibaini ufidadi.

Wafadhili hao - Umoja wa Ulaya (EU) walitoa masharti kwa serikali kutimiza ikiwemo kuchunguza na kushitaki watendaji watakoathibitika kufanya jinai.

Hatua hiyo ya kushitaki watendaji serikalini haikutekelezwa, lakini baadaye kulifanyika marekebesho kwa gharama za serikali yenyewe ndipo wafadhili walipokubali kurudi kuendelea kufadhili.

Mradi huo ulikamilika baada ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kutoa zaidi ya Sh. bilioni 2.5 za kumlipa mshauri wa kuangalia upya michoro ya mradi huo.

Akiwa katika siku ya kwanza ya



ziara maalum ya kutembelea miradi ya maendeleo inayohusisha fedha zilizotolewa kama mkopo kutokana na kupunguza athari za Covid 19, Rais Dk. Mwinyi alimfukuza mkandarasi aliyejiridhisha kuwa ameshindwa kazi.

Aliagiza mkandarasi wa mradi wa Skuli ya Munduli, Wilaya ya Magharibi A, Unguja, aitwaye Associate Construction Company afunge virago na kuondoka. Alipewa kazi ya kujenga jengo la ghorofa tatu la madarasa 41 na vyoo vya kisasa 44 na kazi ikamilike kwa miezi sita. Mpaka anafukuzwa Julai 16, 2022, alikuwa anamalizia ghorofa ya kwanza, akiwa ameanza kazi Machi mwaka huu.

Kwa sababu amebaini udhaifu kwa hata mtaalamu mshauri, Rais pia aliagiza mshauri huyo aiache kandarasi. Huyu ni Edge Consultancy, ambaye Rais anasema hakuwajibika kwa kutoieleza mapema serikali kuhusu tatizo la mkandarasi.

Rais Dk. Mwinyi ameridhika na miradi ya afya na kumsifia waziri wake, Nassor Ahmed Mazrui akisema anafanya kazi nzuri ya kusimamia. Akijua kuwa waziri huyo anatoka chama mshirika katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa - ACT Wazalendo - alisema “anafanana kiutendaji wa wale wa CCM,” kauli iliyozua mguno kwa kuwa chama chake ndio wasimamizi wa miradi inayokusasua.

Tutakumbuka Daima...



KWAMBA Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa kwanza wa Tanzania, alifanya ziara nchini Uingereza Juni 21, 1975, ambapo usiku wa tarehe hiyo aliandaliwa hafla kwenye Hoteli ya Claridge, jijini London. Hafla hiyo ilihudhuriwa na wakuu wa nchi hiyo. Katika picha - Mwalimu akizungumza na Malkia Elizabeth II. (Picha kutoka Maktaba ya Pambazuko).

Salamu zisizokuwa rasmi



Na Dkt. Michael Mashauri

KISWAHILI ni miongoni mwa lugha zinazokua kwa kasi kubwa kila siku duniani. Vyuo vikuu nje ya Afrika, vimeanza kufunza lugha hiyo adhimu. Kutokana na umuhimu wake, Pambazuko limeamua – kila wiki, kuwa njia ya kufundisha Kiswahili bure kwa yeyote anayependa.

Leo Mwalimu anazungumzia juu ya salamu zisizokuwa rasmi (informal greetings) za lugha hiyo.

Salamu zisizo rasmi hutumika katika miktadha isiyo rasmi. Hutumiwa zaidi na vijana katika mazungumzo yao ya kila siku. Wakati fulani huweza pia kutumiwa na watu wazima. (Informal greetings are used in informal contexts. They are mostly used by youth in their daily conversation. They can sometimes also be used by elders.)

Mifano (Examples)

Shangwe: Mambo Juma

(How are things Juma)

Juma: Poa Shangwe (cool [fine] Shangwe)

Shangwe: Vipi nyumbani? (How is home?)

Juma: Shwari kabisa (So peaceful/fine?)

Shangwe: Sawa, baadaye basi (Okay, see you later)

Juma: Poa (fine)

Other informal greetings and their responses:

A: Salama? (How is it/How are you?)

B: Salama (It is okay/ I am fine)

A: Mzima? (Are you okay/ fine?)

B: Mzima (I am fine/good/okay)

A: U hali gani? (How are you -

what is your condition?)

B: Mzima/salama/safi (I am fine/good)

A: Vipi? (Hi/What's up?)

B: Poa / shwari / salama (Hi/Cool/okay/good)

A: Uko poa? (Are you okay?)

B: Niko poa (I am cool/fine/okay)

A: Kwema? (How is there? How are you doing?)

B: Kwema (Fine)

Salamu hizi huweza kuambatana na kupungiana au kushikana mikono. Huweza pia kuambatana na maneno yanayoonyesha mahusiano ya wanaosalimiana. (These greetings may be accompanied by shaking or waving hands. They can also be accompanied by names that identify their relationships). Mifano (example):

Boys to boys

A: Mambo vipi mwanangu? (How are you my friend?)

B: Shwari tu mwanangu (I am fine my friend)

A: Sema jembe (Hi guy)

B: Mzuka (Hi/ I'm so strong/fit)

A: Vipi washikaji? (Hi guys/friends)

B: Poa mwana (It is okay friend)

Girls to girls

A: Habari shoga yangu (How are my friend?)

B: Nzuri/sijambo shoga (I am fine my friend)

A: Mambo mpenzi! (How are things friend?)

B: Poa mpenzi (I am good friend)

• Mwandishi wa Darasa la Kiswahili ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Nguvu ziongezwe kuimarisha sekta ya uziduaji



Waziri wa Madini, Dotto Biteko

Na Moses Msofe

ONGEZEKO la shughuli za kibinadamu, ukuaji wa teknolojia katika maeneo yenye rasilimali nyingi, ni baadhi ya vitu ambavyo vinatajwa kuja na athari mbalimbali kwa mazingira, uchumi na maadili.

Kwa kulitambua hili, serikali ya Tanzania iliandaa utaratibu ambao unatajwa kurahisisha utendaji kazi wa wawekezaji na wakati huohuo kutoa majibu kwa athari zinazotokana na shughuli zao. Utaratibu huo ulipewa jina la “Uwajibikaji wa Mashirika/Kampuni kwa Jamii”

Baada ya utaratibu huo kuonekana kuwa na majibu chanya katika kutatua athari zitokanazo na uwekezaji, serikali ilianza kuurasimisha utaratibu huo kwa kuuingiza kwenye sheria zake na kuufanya kuwa hatua za lazima kwa kila mwekezaji.

Sekta ya uziduaji Tanzania inatambua

na ilisharasimisha utaratibu huu katika sheria zake mbalimbali. Mfano; Sheria ya Uziduaji (2015), Sheria ya Udhhibiti Mazingira (2004), Sheria ya Madini (2019) na nyingine.

Kifungu namba 105 cha Sheria ya Madini (2019), kimeainisha mambo kadhaa yanayotakiwa kutekelezwa na mwekezaji katika sekta hii kuhusiana na uwajibikaji kwa jamii.

Mambo hayo ni pamoja na; Kila mwaka mmiliki wa leseni ya madini ataandaa mpango wa uwajibikaji kwa jamii kwa kushirikiana na halmashauri husika, mpango huo utapitishwa na halmashauri kwa kushirikiana na wizara inayohusika na serikali za mitaa na wizara ya fedha.

Pia inaelezwa kuwa mpango huo uzingatie masuala yote ya kutunza mazingira, kijamii na kiutamaduni ambayo ni vipaumbele vya halmashauri ya jamii mwenyeji.

Zaidi, halmashauri husika zinapaswa kusimamia utekelezaji wa mpango huo pamoja na kujulisha jamii juu ya miradi inayohusishwa na mpango huo.

Hata hivyo, pamoja na kuwepo kwa taratibu hizo, bado kuna maswali kadhaa ambayo sheria imeyaacha bila majibu, maswali hayo ni pamoja - je, kwa nini mipango ya uwajibikaji wa mwekezaji kwa halmashauri iwe ya mwaka mmoja? Je, kampuni zinabanwa namna gani na sheria ili kuhakikisha zinatekeleza wajibu wake kwa jamii?

Hivi karibuni dunia imeshuhudia kampuni ya Anglo Gold Ashanti – mgodi wa Obuasi, nchini Ghana, ikitia saini mkataba wa miaka 10 wa uwajibikaji kwa jamii. Kwanini wawekezaji wa Tanzania nao wasilazimishwe kufanya hivyo.

Pia ni muhimu kwa umma kujua kiwango cha juu cha bajeti zinazotengwa na wawekezaji kwa ajili ya kuwajibika kwa jamii badala ya kuonekana ama kusikika tu mwekezaji akitangaza kutoa “msaada.”

Mpemba: Mtanzania kijana aliyetikisa dunia ya utafiti - 3

KATIKA toleo lililopita, Mtanzania – mwanafunzi wa sekondari, aliyetikisa dunia ya watafiti, Erasto Bartholomeo Mpemba, kwa kugundua kuwa maji ya moto huganda haraka zaidi kuwa barafu kuliko maji yenye ubaridi. Sasa endelea na sehemu ya mwisho ya makala haya...

Na Ally Mahadhy

Dkt. Osborne aliporudi Dar es Salaam aliorudia ule utafiti, kwa kuweka maji ya moto na baridi kwenye 'bikari' mbili tofauti, kisha akaziweka kwenye jokofu kwa muda wa saa moja. Majibu aliyopata ni kama yale aliyoyapata Mpemba; kwamba maji moto huganda haraka zaidi kuliko maji baridi yanapowekwa kwenye jokofu.


Kwa kutumia ufahamu wake kwenye Fizikia, pamoja na utafiti aliouhuhudia, kama ilivyokuwa kwa Mpemba, aliamua kuungana na mwanafunzi wake kuandika andiko ambalo lilichapishwa kwenye jarida maarufu la watafiti la mwaka 1969.

Katika jarida hilo la 'Journal of Physics Education' lenye kichwa cha habari; Cool? Waandishi hao walieleza ukweli wa utafiti ulioanza kwa kijana wa Kitanzania, Erasto Mpemba tena akiwa sekondari.

Baadhi ya vyanzo vya kitafiti duniani vimeainisha kwamba "Mpemba Effect" ni moja kati ya 'falsafa chache za Fizikia' iliyopewa jina la mtafiti wa kiasia.

Kwa kuona umuhimu mkubwa wa "Mpemba Effect" katika ulimwengu huu wa sayansi na teknolojia, mwaka 2012, jarida la 'The Royal Society of Chemistry' la Chuo Kikuu cha Cambridge cha Uingereza, lilitangaza zawadi nono ya pesa kwa mtu au kikundi cha wanasayansi watakaoweza kutoa maelezo mazuri, bora na ya kujenga zaidi kuhusu "dhana" kwamba maji ya moto yanaganda haraka zaidi kuliko maji ya baridi - "Mpemba Effect".

Watu zaidi ya 22,000 walijitokeza, kisha 11 wakaingia fainali, na hatimaye Nikola Bregovic kutoka Croatia ambaye ni mfanayakazi wa Maabara ya Kemia katika



Erasto Bartholomeo Mpemba

Chuo Kikuu cha Zagreb, akatangaza kwa mshindi.

Januari 10, 2013 Mtanzania Erasto Bartholomeo Mpemba ndiye aliyepewa heshima kubwa ya kumtangaza mshindi na kumpa zawadi hiyo kwa niaba ya Jarida la 'The Royal Society of Chemistry', tukio ambalo lilichochea hamasa juu ya udadisi, utafiti na ugunduzi kwa vijana wengi wa nchi za Ulaya na Marekani.

"Mpemba Effect" iko bado na inaishi kwenye maabara mbalimbali duniani, kuanzia Ulaya, Amerika na Asia, lakini siyo Tanzania. Tafiti mbalimbali zimeshafanywa na bado zinaendelea kufanywa ili kutafuta sababu za msingi za "dhana" hii ili mwishowe ize kuwekwa katika matumizi sahihi kama kanuni (law) kwa ajili ya maendeleo ya binadamu.

Rai ya mhariri: Taarifa zilizotufikia hivi karibuni zinaeleza kuwa Erasto Mpemba alifariki dunia mwaka 2020 na kuzikwa kwa Songea.

***Mwandishi wakati akiandika makala haya alikuwa mwanafunzi wa Tanzania akisoma shahada ya uzamivu katika Chuo Kikuu cha Lund, Sweden.**

Uzuri, ubaya wa simu za mkononi

Na Yusuf Jumah, BBC Swahili

SIMU ya mkononi au rununu ni kifaa kidogo chenye athari kubwa kwa maisha ua binadamu na kwa wanaokitumia vizuri, manufaa yake ni makubwa pia .

Dunia ya teknolojia inamaanisha kwamba matumizi ya simu ya mkononi ni jambo la kawaida na kila mwaka mamilioni ya watu wanaingia katika kundi la wanaoanza kutumia simu hizo.

Hata hivyo, matumizi ya simu za mkononi yanakuja na madhara yake ambayo mwanzoni watu wengi hawakuwa wakijua yanaweza kuvuruga maisha yao, siyo tu kiafya pekee, bali pia kisaikolojia na hata kuhatarisha maisha yao .


Iwapo hukujua kwamba simu hiyo ya mkononi unayotumia kila siku inaweza kuyavuruga maisha yako -hizi hapa njia nne ambazo unaweza kujipata pabaya endapo hutakuwa muangalifu au makini kuhusu matumizi yako ya simu .

Simu inaweza 'kubadilisha tabia yako kijamii': Kuna ushahidi wa wazi ambao wanaoikolojia wanasema matumizi ya simu yanaweza kuleta kwa tabia ya mtu hasa kijamii. Siyo jambo la ajabu kujua kwamba kwa sasa kuna watu, hasa vijana ambao matumizi ya simu yameathiri sana uwezo wao iwe shuleni au kazini.

Hilo hutokana na mazoea ambayo iwapo hayaangaliwi yanaweza kuwa uraibu unaovuruga kabisa jinsi mtu anavyotangamana na wengine kijamii.

Kutumia simu ukiendesha gari au ukifanya kazi inayohitaji umakinifu: Umesikia kuhusu ajali za barabarani zinazosababishwa na madereva ambao wanaendesha gari wakitumia simu za mkononi. Takwimu ni nyingi kuhusu idadi ya maafa yanayosababishwa na ajali kama hizo .

Kwa muda mrefu watu wamekuwa wakitumia simu kama kinga ya kufanya maovu na uhalifu. Sheria zinabadilika na kuboreshwa na usije ukadanganyika



Matumizi makubwa ya simu ni hatari.

kwamba unaweza kutekeleza uhalifu kutumia simu yako ukifikiri uko salama.

Nchini Kenya kwa mfano, mwanamke mmoja yupo mashakani kwani huenda akafungwa jela kwa kutoa shilingi 271,200 alizotumiwa kimakosa katika akaunti yake ya Mpesa kupitia simu .

Hakikisha unanunua simu yako kwa njia halali ama kwa muuzaji mwenye leseni: Iwapo ulifikiri unaweza kuinunua simu ya mkononi kwa yeyote kwa sababu umeipata kwa gharama ya chini, basi itabidi umeliwazia tena suala hilo. Kuna hatari kubwa sana kununua simu kutoka kwa mtu yeyote. Ipo mifano ya watu waliofungwa jela kwa makosa makubwa hata ya mauaji kwa kuuziwa simu ambazo zilipatikana kutumika katika uhalifu

Manara atashinda rufaa?

Na Francis Garatwa

NI haki ya kila mmoja kukata rufaa baada ya uamuzi ikiwa hataridhika; na ni wajibu wa mtoa uamuzi kutoa haki ya mtuhumiwa kukata rufaa kwenye mamlaka ya juu zaidi.

Isipokuwa; haki hiyo ya kukata rufaa kwenye mamlaka nyingine inakuwa na taratibu ambazo ni lazima uzifuate na kuzizingatia kabla ya kuwasilisha rufaa.

Rufaa inaweza kuwa (Judicial Review) kutafuta nafuu nyingine kwenye mamlaka ya juu baada ya kuona kwamba uamuzi husika dhidi yako haukuzingatia taratibu za kisheria ama haukuridhishwa na uamuzi kwa sababu nyinginezo.

Suala la rufaa anayotaka kuikata Msemaji wa Yanga, mabingwa wa soka Tanzania, Haji Manara likiangaliwa kwa jicho la kisheria, linabeba ukakasi kwa sababu taratibu za kisheria na mwenendo wa shauri lake hauko sawa.

Pamoja na kwamba hati ya rufaa haijawekwa hadharani; kama anapinga hoja ya kupatikana na hatia mbele ya mamlaka ya uamuzi, itakuwa vigumu kushinda rufaa hiyo na anaweza kujikuta anaongezewa adhabu.

Isipokuwa kama anakata rufaa kwa maana ya kuomba kupunguziwa adhabu aliyopewa ya miaka miwili na faini ya Sh. 20,000,000 (milioni ishirini), hiyo itategemea na busara za mamlaka ya rufaa yake, lakini pia hoja atakazoainisha wakati akiomba punguzo la hiyo adhabu.

Ilishangaza kwa Manara - kwa makusudi ama kwa kutojua, kujivika kitanzi kwenye shauri hili kwa kuomba radhi hadharani tena mbele ya vyombo vya habari, lakini pia inaelezwa kuwa aliwafata viongozi wa Shirikisho la Soka (TFF) kuwaomba radhi ana kwa ana.

Kibaya zaidi wakati wa kuomba radhi hadharani, alimtaja mlalamikaji kwa majina yake halisi yaliyotajwa kwenye shauri yaani Wallace Karia.

Lakini, pia alitaja wadhifa wa mlalamikaji (Rais wa TFF) hadharani



Msemaji wa Yanga, Haji Manara

kama ulivyotajwa kwenye nyaraka za shauri hili na akawa kumbukumbu kwenye vyombo vya habari.

Ikiwa Manara na timu yake ya wanasheria wanakata rufaa kwa kupinga kupatikana na hatia, ni lazima waanze kwa kuyakana kisheria maombi yote ya kumuomba radhi Wallace Karia na hatua yake ya kuiomba radhi TFF.

Akiamua kuyakana kisheria maombi haya ya kuomba radhi yaliyofanyika hadharani, atambue ni mchakato wenye mlolongo wa kumtoa mtu jasho.

Ushauri pekee anaoweza 'kuukumbatia' sasa Manara ni 'kutuliza akili' - asiendelee kutoa kauli zenye ukakasi dhidi ya mamlaka za uamuzi kwa lengo la kuwafurahisha wafuasi na mashabiki kwa sababu tayari yupo ndani kipindi cha adhabu yenye athari kwa maisha yake binafsi, wategemezi, timu yake na wapenzi wa soka.

PICHA KUBWA

Mkurugenzi Mtendaji wa Timu ya Simba ya Dar es Salaam, Barbara Gonzalez – kamusi yake ya maisha haina neno “haiwezekani.” Anajiamini na kupenda anachofanya. Hapendi kushindwa. Anapenda kujifunza zaidi kutoka kwa wengine. Ni mwanadada aliyekwaa ukurugenzi ndani ya bahari iliyojaa wanaume – mchezo wa soka, akiwa na miaka 30 tu. Kama yeye ameweza, wewe dada unashindwa nini? Jiamini, nawe unaweza. Pichani, Barbara akikumbatiwa na Rais wa Uganda, Yoweri Museveni walipokutana katika Hoteli ya Serena, Uganda mwaka juzi. (Picha: Twitter).



GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi na Habari Tanzania (TAMPA). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

